**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Mkuu wa Shule 0755 451651/0622336398**

**Makamu Mkuu wa Shule 0762280281**

**Matron/Patron 0756164935/0625724706**

**Shule ya Sekondari Iwalanje**

**S.L.P 1217**

**MBEYA**

**Tarehe ....................……………**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI IWALANJE HALMASHAURI YA WILAYA MBEYA MKOA MBEYA MWAKA 2023/2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya …………

Shule ya Sekondari Iwalanje ipo umbali wa Kilometa 12 Kusini mwa mji mdogo wa Uyole. Usafiri wa basi kutoka Uyole unapatikana katika kituo cha mabasi Nanenane Nauli ni Shilingi 1500 kwa basi (panda mabasi yaendayo Tukuyu/Kyela na kushuka stand ya Iwalanje) na Shilingi 1000 kwa pikipiki kutoka Iwalanje hadi shuleni.

Muhula wa Masomo unaanza 14/08/2023, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13/08/2023 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/08/2023

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni suruali *dark blue* na kijani kibichi kwa Wavulana pamoja na shati mbili nyeupe mikono mirefu, Tai *dark blue* na kijani kibichi.
ii. Mshono wa suruali ni mifuko ya pembeni, Rinda mbili upande wa mbele na turn up kwa mkunjo wa chini.

iii. Sare ya michezo kwa shule hii ni *Track Suit* moja (*Right blue*)
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi mbili nyeusi;
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
vii. Sweta moja ya kijani iliyoshonwa vizuri yenye shingo V
viii. Nguo za kushindia *TRACK SUIT* moja nyeusi
ix. Tai rangi ya *dark blue* na kijani kibichi.
x. Tisheti (T-shirt) (zinapatikana jirani na shuleni).
xi. Koti au sweta zito kwa ajiri ya baridi (litavaliwa baada ya masomo)

## 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari counter book 15 za quire 3
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
iv. Scientific Calculator;
v. Godoro Godoro kwa wanafunzi wa bweni futi 2 ½
vi. Mashuka pair 2 rangi ya pink, blanketi 1, Foronya 1
vii. Nguo za ndani za kutosha;
viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
ix. Ndoo 2 kubwa 1 ndogo 1 zenye mifuniko;
x. Kwanja 1, jembe 1 lenye mpini lililo nolewa, reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje pamoja mopa 1.
xi. Spring file moja

**NB**: Mwanafunzi aje na bima ya afya kwa ajili ya matibabu

## 2.3 Michango mbalimbali

### a) Shule za Bweni

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB. Fedha zote zilipwe kupitia beki NMB , Acc 61001200136, Iwalanje sekondari**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;

xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
ii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iii. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ……………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule …………………………………….**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0755451651**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0784236613**
- **Mwandamizi Taaluma 0755041302**
- **Mwandamizi Malezi 0756164935**

**MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY**

IWALANJE SECONDARY SCHOOL,

P.O. BOX 1217,

MBEYA.

DATE: .....................................

MEDICAL OFFICER

GOVERNMENT HOSPITAL

P.O. BOX ........................

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Please examine ................................................................................... (Student) as to her/his fitness

For pursuing further Education at this school

**.............................................**

**HEADMASTER**

1. Haemoglobin .......................................................................................................................
2. P.V. Bleeding .......................................................................................................................
3. Blood pressure .......................................................................................................................
4. Blood Group .......................................................................................................................
5. (a) Sight .......................................................................................................................

   (b) Hearing .......................................................................................................................
6. Urine for sugar and pregnancy test .......................................................................................
7. Stool for routine – Examination .......................................................................................
8. Athma .......................................................................................................................
9. Skin diseases .......................................................................................................................
10. Epilepsy.......................................................................................................................
11. Leprosy .......................................................................................................................
12. Pulmonary tuberculosis.......................................................................................................

13. Deformity.......................................................................................................................

14. Mental problems.................................................................................................................

15. V.D. (Give type)..................................................................................................................

16. Any other serious disease not mentioned above.........................................................................

.......................................................................................................................................

OTHER COMMENTS: ..........................................................................................................

..................................................................................................

**DESIGNATION AND SIGNATURE………………………………………………………….**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**

**SHULE YA SEKONDARI IWALANJE**

**FOMU YA KUKUBALI:**

1.SEHEMU YA KWANZA

Mimi…………………………………………………………………..ninakubali nafasi Niliyopewa kuingia kidato cha TANO mwaka……………………… katika shule ya sekondari Iwalanje na nitafika shuleni bila kuchelewa. Ninaahidi kwamba nitatii na kuzingatia sheria zote za shule
Na za nchi . Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi ya Elimu ya kujitegemea.

Anwani yangu ya kudumu ni:
………………………………………………………
………………………………………………………
………………………………………………………

2. SEHEMU YA MZAZI /MLEZI:

Mimi…………………………………..……..………ninakubali mtoto wangu……………………………………kuchukuwa nafasi kuingia shule ya sekondari Iwalanje …………….. Kidato cha Tano mwaka ……………….. ninaahidikumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule. Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu kwa shule na Taifa. Anwani yangu ya kudumu ni:

….…………………………

………………………………

……………………………...
Simu Na. …………………

Iwapo nitapata uhamisho au kubadilisha makazi nitaijulisha shule kwa maandishi

Sahihi…………………………………………………………………..
Tarehe………………………………………………………………….

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, NA TEKNOLOGIA**
**SHULE YA SEKONDARI IWALANJE**
**TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1. Jina kamili………………………………………………………………………………

2. Tarehe ya kuzaliwa……………………………………(tarehe, mwezi, mwaka)

3. Kabila……………………………………………..taifa……………………………………

4. Dini na madhehebu………………………………………………………………………..

5. Jina la Baba……………………………………(Namba ya simu)…………………………..

7. Kazi ya Baba……………………………………………………………………..

8 .Jina la Mama………………………………Kazi yake……………… Namba ya simu……………………

9. Wazazi wanaishi pamoja au wametengana…………………………………………………

10. (a)Jina la mlezi aliyeko mkoa wa Mbeya…………………………………………..

(b) Kama ni mlezi uhusiano wako naye…………………………………………….

(c) Anwani ya mlezi……………………………………………….. Namba ya simu……………………………………………..

11. Wakati wa likizo utakuwa kwa nani? (Taja sehemu moja tu utakayo kwenda kila wakati. Anwani)………………………………………………………………………………

12. Nathibitisha kwamba habari zote nilizotoa ni za kweli na sahihi.

Sahihi ya mwanafunzi………………………………………Tarehe………………………….

Sahihi ya mzazi/Mlezi………………………………………Tarehe…………………………

OFISI YA MKUU WA MKOA,
MKOA WA……………………,
WILAYA………………………,
S.L.P……………..,

MKUU WA WILAYA,
…………………………………………..
…………………………………………..
…………………………………………..

**UTHIBITISHO WA URAIA WA TANZANIA**

Nathibitisha kuwa…………………………………………………(Jina kamili la Mwanafunzi) ni raia wa Tanzania kwa kuzaliwa/kwa kuandikishwa.

Baba yake (jina kamili)……………………………………………………….

Amezaliwa katika Mkoa wa……………
………………………………. Wilaya ya………………………………………………

Tarafa ya………………………………kata ya…………………………………………

Mama yake(jina kamili)………………………………………………………………

Amezaliwa katika kata ya ………………………..Wilaya ya……………………………….

Mkoa wa ……………………………………………………

**……………………………….**
**MKUU WA WILAYA**

**NB; MWANAFUNZI KAMA HANA CHETI CHA KUZALIWA NI LAZIMA FOMU HII IJAZWE KWA MKUU WA WILAYA HUSIKA AU NAKALA YA CHETI CHA KUZALIWA KIWASILISHWE SHULENI BADALA YA FOMU HII**